

Katibu tawala mkoa wa Dodoma **Bw. Ally Gugu** amekagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo Jana tareh 4 ,mei 2023 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na kuangazia miradi katika sekta ya Elimu ,Afya na Utawala.

Bwana Gugu ametembelea miradi Saba ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la Halmashauri,Nyumba ya mkurugenzi na ujenzi wa nyumba tatu za watumishi,miradi mingine ni hospitali ya Halmashauri ya Wilaya iliyoko Bukulu ,ujenzi wa ukuta katika shule ya kulelea watoto wenye maalum iliyoko katika kijiji cha **Bereko** pamoja ujenzi wa madarasa na chumba maalum cha kujifunzia kompyuta shule ya msingi Isabe .

Katika ziara yake bwana Gugu ametoa Rai Kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Bw. Mustafa Semwaiko Yussuf kuhakikisha miradi yote inayoendelea kutekelezwa katika hatua mbalimbali iweze kukamilika ifikapo tarehe 31mei 2023.

Serikali imetoa sh bil 1.2 kuwezesha ujenzi ofisi na makao makuu ya Halmashauri Bukulu na ujenzi wa nyumba 3 za wakuu wa idara.Aidha katika sekta ya Afya Bw.Gugu amepongeza hatua nzuri ya maendeleo ya ujenzi wa majengo manne katika hospitali ya Halmashauri ambayo ni wodi ya wanaume, wanawake, watoto pamoja jengo la kuhifadhi maiti ambavyo gharama yake ni mil 750 kutoka serikali kuu.

Pia Bw. Gugu amepata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa jengo la computer (CLUSTER)na ujenzi wa madarasa katika shule ya msingi Isabe ambavyo gharama yake ni mil 80. Kufuatia ukaguzi huo wa miradi ya sekta ya Elimu, Afya na Utawala Bw.Gugu ametoa maelekezo ya kuhakikisha kuwa miradi yote inakamilika Kwa muda uliopangwa na Kwa ubora wa Hali ya juu.

"Niwahakikishie kuwa tutarudi tena haya maelekezo tuliyowapa yazingatieni na tutakaporejea tupate taarifa ya utekelezaji wake Kwa vitendo "alisisitiza Gugu.

Pia Bw. Gugu amepata fursa ya kuzungumza na watumishi wa Halmashauri na kuwaasa kufuata misingi na taratibu za utumishi wa umma na kusisitiza kuacha kufanya kazi Kwa mazoea na kila mtumishi kuzingatia mambo makuu manne ambayo ni ,**“Kuheshimiana mahali pa kazi,Uadilifu kazini na mali za umma na mwisho ni kujituma zaidi ili kutimiza azma ya serikali mwisho wa kunukuu“**